

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI TARIME**

Simu: +25528-2690218
+255282690043
Nukushi: +25528-2690218
Barua pepe: td@tarimetc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji
S.L.P 45'
TARIME

ZABUNI NA: LGA/165/2018/2019/S/O1

KWA AJILI YA:

**UPIMAJI WA VIWANJA 1238 ENEO LENYE UKUBWA WA EKARI
545 KATA YA NYANDOTO HALMASHAURI YA MJI TARIME**

MARUDIO YA MWALIKO WA ZABUNI

Tarehe 20 Februari, 2019

Kwa:.....
.....
.....


- 1. Halmashauri ya Mji Tarime S.L.P 45 Tarime** imetenga Fedha kwa ajili ya uendeshaji wa **Halmashauri ya Mji Tarime S.L.P 45 Tarime** katika mwaka wa fedha **2018/2019**. Inakusudiwa kuwa sehemu ya Mapato ya fedha hizo yatatumika kugharimia malipo halali ya mkataba ambao utatolewa kutokana na Mwaliko wa Zabuni hii ambao ni **Upimaji wa Viwanja 1238 Eneo lenye Ukubwa wa Ekari 545 Kata ya Nyandoto Halmashauri ya Mji Tarime**.
- 2. Unakaribishwa** kuleta maombi yako yenye bei kwa ajili ya kufanya kazi tajwa hapo juu kama ilivyoelezwa kwenye Orodha ya Mahitaji na Bei na kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya II.

S/N	Maeleza ya kazi	Kazi
01	Upimaji wa Viwanja 1238 Eneo lenye ukubwa wa Ekari 545 Kata ya Nyandoto Halmashauri ya Mji Tarime.	Upimaji wa Viwanja 1238 eneo lenye ukubwa wa Ekari 545.

- Zabuni zote ziwe na nakala halisi (original) moja na nakala mbili zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu. Juu ya Bahasha iandikwe "Zabuni Na. LGA/165/2018/2019/S/01 kwa ajili ya Upimaji wa Viwanja 1238 Eneo lenye ukubwa wa Ekari 545 Kata ya Nyandoto Halmashauri ya Mji Tarime. Ni lazima kupelekwa kwa Mkurugenzi wa Mji Tarime S.L.P 45 Tarime, Ofisi ya Kitengo cha Manunuzi.
- Siku ya mwisho ya kuwasilisha Zabuni hii ni Siku ya **Jumane Tarehe 05/Machi/2019** muda wa **Saa 8:00 Mchana katika Ofisi ya Kitengo cha Manunuzi Halmashauri ya Mji Tarime.** Zabuni zote zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, mbele ya wawakilishi wa wazabuni walioamua kuhudhuria katika kikao cha ufunguzi wa zabuni katika **Halmashauri ya Mji wa Tarime S.L.P 45 Tarime.**
- Kitabu cha zabuni kitakuwa kwa Lugha ya Kiswahili na kitauzwa kwa ada ya gharama ya **Tsh.100,000** Fedha ambayo haitarudishwa (**Non-Refundable fee**). Malipo ni lazima yafanyike kupitia **NMB Bank Tawi la Tarime kwa akaunti Na.30410005254.** Kumbuka Malipo haya yatalipwa baada ya kupata Ankara ya Malipo (Bill of Payment) kutoka ofisi ya Idara ya Fedha Kitengo cha Mapato Halmashauri ya Mji wa Tarime.
- Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya kotesheni, Zabuni za kielektroniki, na Zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguzi wa Zabuni, kwa hali yoyote ile hazitakubaliwa kwa tathmini. Tangazo la Zabuni hii pia unaweza kulipata katika website ya Halmashauri ya Mji Tarime www.tarimetc.go.tz, na ppra portal (Journal),

Nawasilisha


 ELIAS R. NTIRUBUNGWA
 MKURUGENZI WA MJI
 HALMASHAURI YA MJI WA TARIME


 MKURUGENZI MTEGAJI
 HALMASHAURI YA MJI WA
 TARIME